Sikika

Jarida la Sikika

Namba ya Usajili 00005809 Toleo 24: Disemba, 2016

Huduma Bora za Afya kwa Wote

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mh. Ummy Mwalimu akifanunua jambo katika mkutano wa Wadau wa Sekta ya Afya nchini. Kulia ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mh.Selemani Jafo na Kushoto ni Katibu wa Wizara hiyo Dkt. Mpoki Ulisubisya. Wengine pichani ni Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI – Afya Dkt. Zainabu Chaula na Mkurugenzi wa Sikika Bw. Irenei Kiria.

Utangulizi

KARIBU kwenye Jarida letu la 4, toleo la 24 ili uweze kufahamu muhtasari wa shughuli zilizofanywa na Sikika katika robo ya nne ya mwaka (2016).

Tulitekeleza kazi mbalimbali kwa lengo la kuhimiza uwajibikaji katika uboreshaji wa mifumo ya afya na usimamizi wa fedha.

Utekelezaji wa zoezi la Ufuatiliaji na Uwajibikaji kwa Jamii (UUJ/SAM), wilayani Kilolo umeleta matokeo chanya baada ya timu ya UUJ/SAM kwa kushirikiana na viongozi wao, wameanza kuhimiza dhana ya uwajibikaji kwa wananchi na watoa huduma wilayani humo. Pia, baadhi ya changamoto zilizoibuliwa wakati wa kufuatilia upatikanaji huduma na utekelezaji wa miradi ya afya, zimeanza kupatiwa ufumbuzi.

Katika kipindi hiki, Sikika ilishiriki kwenye mkutano wa mwaka wa wadau wa sekta ya afya nchini. Lengo la mkutano huo lilikua ni kutathmini maazimio ya kisera ya sekta ya afya kwa mwaka 2017/2018, ili kuboresha utolewaji wa huduma za afya nchini.

Pia, shirika lilibaini jinsi zoezi la uhakiki kwa utumishi wa umma nchi nzima lilivyoathiri upatikanaji wa huduma za afya hususan maeneno ya vijijini. Katika baadhi ya maeneo, watumishi wa afya waliitwa kufanya uhakiki kwenye makao makuu ya wilaya na kukaa nje ya vituo vyao vya kazi kwa muda mrefu, hali iliyozorotesha upatikanaji huduma za afya.

Unaweza pia kupata taarifa zaidi kuhusu kazi za Sikika kupitia tovuti yetu; *www.sikika.or.tz, twitter- @sikika1, facebook- Sikika Tanzania na blogspot - www.sikika-tz.blogspot.com.* Kwa maoni tafadhali wasiliana nasi kupitia *info@sikika.or.tz* au sms *0688-493- 882.*

NDANI

UTANGULIZI 1
Ushirikiano Nguzo Muhimu Kutekeleza Sera ya Afya -2017 2
Uhakiki Watumishi Usiathiri Huduma za Afya.....3
SAM Yaleta Matokeo Chanya 4

HALIUZWI

Ushirikiano Nguzo Muhimu Kutekeleza Sera ya Afya -2017

Na Beatrice Mkani

"Ushirikiano! Ushirikiano! Ushirikiano!" Alisikika akihimiza Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Mpoki Ulisubiya katika mkutano wa kisera wa sekta ya afya uliofanyika Desemba 7, mwaka 2016. Mkutano huu ulikuwa na lengo la kujadili maazimio ya kisera ya sekta ya afya kwa mwaka 2017/18, ili kuboresha utolewaji wa huduma za afya nchini.

Katika mkutano huo, serikali ilisisitiza ushirikiano mkubwa wa wadau mbalimbali wa sekta ya afya katika kufanikisha mipango iliyoweka ya kuendelea kuyapa kipaumbele maeneo makuu manne ya afya yaliyopo katika mpango mkakati wa 2015/20. Maeneo hayo ni; Rasilimali watu katika sekta ya Afya, Dawa na vifaa tiba, uendeshwaji na usimamizi wa vituo vya afya pamoja na afya ya uzazi, mama na mtoto.

"Tumeona jinsi ushirikiano ulivyotufikisha, hata hizi sera za mwaka huu zimetokana na ushirikiano, hivyo tutaendela kushirikiana na wadau wote mliopo hapa katika utekelezaji wa sera kwa mwaka ujao"- Aliunga mkono Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Bi. Ummy Mwalimu.

Katika mkutano huo, Sikika iliziwakilisha asasi za kiraia zinazofanya kazi katika sekta ya afya, chini ya mwavuli wa Policy Forum na ilipata fursa ya kusoma tamko kwa niaba ya asasi hizo. Mambo makuu manne muhimu katika kuboresha huduma za afya nchini yaliainishwa katika tamko hilo. Kwanza ni changamoto za upatikanaji wa taarifa muhimu katika utekelezaji wa kazi za taasisi za kiraia. Ilielezwa kwamba kumekuwa na ugumu wa baadhi ya taarifa kupatikana, jambo ambalo linapunguza ufanisi wa taasisi hizo katika kutoa mchango wao kwa sekta ya afya.

Pili ni upatikanaji wa dawa na vifaa tiba ambapo imeonekena kuwa bado ni tatizo sugu linalowakabili wananchi licha ya serikali kuongeza bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/17. Katika hili, wadau walipendekeza kuwe na suluhisho la kudumu ili tatizo hili lisijirudie mara kwa mara.

Jambo la tatu, ni upungufu wa rasilimali watu katika sekta ya afya. Upungufu huo unatajwa kuchangiwa na kuwepo kwa wahitimu 20,000 ambao wanasubiri kuajiriwa kwa takribani miaka miwili sasa. Aidha, upungufu huo ulielezwa kuwa umesababisha takriban vituo vya afya 2,000 kuendeshwa na watumishi ambao kiwango chao cha taaluma hakikidhi kusimamia vituo. Hivyo, Sikika, kwa niaba ya wadau wa afya, ilipendekeza ajira kwa watumishi wa sekta ya Afya ipewe kipaumbele mwaka ujao wa fedha.

Jambo la nne lilikuwa ni kuboreshwa kwa bima za afya nchini. Licha ya juhudi za serikali kuhimiza uwepo wa mfuko mmoja wa bima ya afya nchini, bado wananchi wanaojiunga katika mifuko iliyopo kama mfuko wa afya ya jamii (CHF) ni wachache na baadhi ya waliojiunga pia wanajitoa kutokana na sababu mbalimbali. Sikika kwa niaba ya wadau wa afya, ilipendekeza kuainisha changamoto zilizopo katika mifuko iliyopo na kuiboresha kabla ya kuingia katika mfuko mmoja wa bima ambao unategemea sana ufanisi wa mifuko inayotumika sasa.

Akijibu tamko hilo, Waziri Ummy Mwalimu, alieleza kwamba serikali imejipanga kutatua changamoto mbalimbali zikiwemo upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa mwaka 2017/18, kuboresha huduma za Bohari Kuu ya Dawa, mifuko ya bima za afya na ukusanyaji wa mapato katika ngazi ya vituo vya afya.

Kwa upande wa upatikanaji wa takwimu, ilielezwa kwamba serikali iko tayari kushirikiana na wadau wote wa sekta ya afya ili kutatuta tatizo la upatakinaji wa taarifa kwenye ngazi zote. "… naona tukishirikiana vyema tunaweza kutatua sehemu kubwa ya changamoto hizi ambazo ni pamoja na kuboresha uwazi na uwajibikaji", alisema Naibu Katibu Mkuu - Afya, Ofisi ya Raisi, (TAMISEMI) Dr. Zainabu Chaula.

Mkutano huu wa wadau wa sekta ya afya nchini hufanyika kila mwaka kwa lengo la kujadili muelekeo wa sekta kwa upande wa sera. Wadau walioshiriki ni pamoja na washirika wa maendeleo, mabalozi kutoka baadhi ya nchi wahisani, sekta binafsi, wawakilishi wa mashirika mbalimbali yanayo jishughulisha na masuala ya afya, wawakilishi wa taasisi za kidini na za kiraia zinazofanya kazi katika sekta ya afya nchini.

3. Zahanati ya Itaja wilayani Singida, ikionekana kutokuwepo kwa likionesha hakukuwa na utolewaji

Uhakiki Watumishi Usiathiri Huduma za Afya

Na Sophia Nshushi, Singida

Serikali ilitangaza zoezi la kuhakiki watumishi wa umma nchi nzima ili kubaini walio halali na watumishi hewa. Zoezi hilo lilifanyika katika sekta zote na lilipata mwitikio mkubwa toka kwa watumishi. Afya ni moja ya sekta ambayo watumishi wake walifanyiwa uhakiki juu ya uhalali wao katika taaluma hiyo ambayo inagusa maisha ya watanzania moja kwa moja.

Pamoja na lengo zuri la zoezi hili, kulikuwa na usumbufu katika upatikanaji wa huduma za afya hasa vijijini. Mfano, baadhi ya watumishi waliohakikiwa walilazimika kusafiri kwenda makao makuu ya wilaya zao na kutumia muda mrefu katika uhakiki, hivyo kuathiri upatikanaji wa huduma za afya hususan katika maeneo yenye uhaba wa watumishi. Baadhi ya vituo vililazimikakusitisha huduma hadi watumishi waliporejea vituoni.

Kutokuwepo kwa utaratibu mzuri wa kuwawezesha watumishi kuhakikiwa bila kuathiri utoaji wa huduma za afya kumeleta usumbufu kwa wagonjwa waliopo katika baadhi ya vituo. Mfano, mnano Tarehe 13/10/2016, Sikika ilitembelea baadhi ya zahanati za wilaya ya Singida na kukuta zimefungwa. Ukutani kulikuwa na tangazo lililosomeka, **"*Tumeenda kuhakikiwa. Poleni*"**

a watumishi kituoni wakati wa saa ya kazi na pembeni ni tangazo wa huduma za afya kituoni hapo.

Wagonjwa waliofika kwa ajili ya kupatiwa huduma walilazimika kurudi nyumbani baada ya kusoma tangazo hilo. Hii ilisabisha usumbufu mkubwa na hasa kwa wagonjwa waliokuwa wanahitaji msaada wa haraka na wale waliotembea umbalimrefu kufuata huduma.

Zoezi la uhakiki halikuathiri wananchi peke yao bali hata watumishi wanaofanya kazi vijijini; "*Ni usumbufu mkubwa sana kwa watumishi tunaoishi maeneo ya vijijni, inatulazimu kusafiri mpaka mjini katika ofisi za halmashauri ili kuhakikiwa, tunatumia siku mbili mpaka tatu tukiwa huko mjini na gharama zote ni juu yetu, hakuna posho ya nauli wala malazi, tunaomba Mkurugenzi wa halimashauri aweze kuongeza masaa ya uhakiki ili kupunguza msongamano wa watu.*"Anaeleza mmoja wa watoa huduma katika moja ya zahanati, wilayani Singida vijijini.

Kaimu Mganga Mkuu Halmashauri ya Singida, Dk. Shani, alifafanua kwamba *"Watumishi huondoka kituoni kutokana na muda mchache uliopangwa wa uhakiki.Na katika baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya, inawalazimu kuondoka wote ili wasichelewe kufanyiwa zoezi hilo.*"

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Singida, Bw. Rashidi Mandoe alikiri kuwepo tatizo hilo. Aliahidi kushughulikia ili angalau muda wakufanya uhakiki uongezwe na kipaumbele kiwe kwa watumishi wa afya, lengo likiwa ni kuepusha usumbufu kwa wagonjwa wanaohitaji huduma.

Zoezi la uhakiki lina lengo la kuleta tija katika sekta zote za serikali ikiwemo Afya. Hata hivyo, tunaomba serikali na mamlaka zinazohusika kuweka utaratibu na mazingira mazuri ili watumishi, hasa wa afya waweze kuhakikiwa bila kuathiri upatikanaji wa huduma stahili kwa wananchi na pia kuwapunguzia watumishi gharama za usafiri na kujikimu.



SAM Yaleta Matokeo Chanya

Na Emmanuel Malongoza, Kilolo

Utekelezaji wa zoezi la Uwajibikaji kwa Jamii (SAM), wilayani Kilolo umeleta matokeo chanya baada ya viongozi kuanza kuhimiza dhana ya uwajibikaji kwa wananchi na watoa huduma wilayani humo.

Baadhi ya mifano chanya imedhihirika pale ambapo waganga wafawidhi na wajumbe wa kamati za vituo vya kutolea huduma za afya walipoanza kusimamia ujenzi wa mashimo ya kutupia kondo la uzazi katika zahanati za Kilolo na Nyanzwa. Ukosefu wa mashimo ya kutupia kondo katika zahanati hizo ni moja ya changamoto zilizobainika kwenye baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya,wakati wa utekelezaji wa zoezi la SAM.

Akielezea mchango wa mafunzo ya uwajibikaji kwa zahanati ya Kilolo, Mwenyekiti wa timu ya SAM ambaye pia ni mjumbe wa bodi ya zahanati hiyo, Bw. John Kasuga alisema “vitu vilivyobadilika ni vingi: kwanza kabla ya SAM kituo hakikuwa na kichomea taka wala shimo la kutupia kondo la uzazi lakini vyote hivi vimetengenezwa mara tu baada ya zoezi la SAM.”

Mifano ya hatua zilizochukuliwa na wana Kilolo ni uthibitisho kwamba baadhi ya changamoto hazihitaji bajeti kubwa bali utashi katika kusimamia mipango na ushiriki wa wananchi.

Changamoto zingine wilayani humo zilizobainika ni uhaba wa nyumba za waganga wafawidhi, ukosefu wa huduma ya maji kwa baadhi ya vituo na kutokuwa na alama za mipaka katika baadhi ya zahanati. Nyingine ni vifaa vinavyotumia nishati ya jua kutofanya kazi kutokana na ubovu/uchakavu, vituo vya mbali na vyenye mazingira magumu kukosa usafiri na uhaba wa watumishi katika sekta ya afya.

Kwa ujumla, Bw. Kasuga anaeleza kwamba mchango wa SAM katika kituo cha Kilolo umewawezesha wananchi kufahamu haki na wajibu wao wa kufuatilia na kuhoji; “Mfano,vile vitu vilivyokuwa havipatikani kwenye vituo kwa sasa baada ya SAM vinapatikana, mfano dawa kutoka bohari ya Dawa na ongezeko la fedha za Mfuko wa hifadhi ya jamii kutokana na ongezeko la watu wanaojiunga ”. Hata hivyo, mjumbe huyo wa timu ya SAM anasema wakati wa kutimiza jukumu lake kama mwananchi, anakumbana na changamoto; “mara nyingi wahudumu wanakuwa na wasiwasi sana kuhusu kuhoji kwangu kwamba labda nakuwa kama mkaguzi, hiyo ni changamoto ninayoipata sana.”

Changamoto nyingine aliyoigusia ni upatikanaji wa taarifa na baadhi ya watendaji kutokuwepo hivyo inasababisha kutopata baadhi ya taarifa. “Kwenye kituo unakuta wahudumu wanakuambia huyu hayupo, mfano anayehusika na mahesabu hayupo, bila kuzingatia kuwa inatakiwa kwenye kituo kama mfanyakazi akiondoka ni lazima akabidhi taarifa za muhimu”.

SAM inaweza kuleta mabadiliko makubwa iwapo itakuwa endelevu, itashirikisha wanajamii pamoja na timu ya SAM. Bw. Kasuga anatoa wito kuwa, “timu ya SAM iiendelee tu,iwe ni timu ambayo ni endelevu isiwe ya muda, kwa sababu inaleta mabadiliko makubwa sana kwenye vituo.”

Wajumbe wa timu ya SAM wilayani Kilolo wakikagua baadhi ya nyaraka katika zoezi la SAM lililofanyika wilayani humo.

Sikika

Nyumba Na. 69
Ada Estate, Kinondoni
Barabara ya Tunisia
Mtaa wa Waverley
S.L.P 12183 - Dar Es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 26 663 55/57
Ujumbe Mfupi: +255 688 493 882

Nukushi: +255 22 26 680 15
Barua Pepe: info@sikika.co.tz
Tovuti: www.sikika.or.tz
Blog: www.sikika-tz.blogspot.com
@sikika1
Sikika Tanzania
sikikatanzania

Nyumba Na. 340
Mtaa wa Kilimani
S.L.P 1970
Dodoma, Tanzania
Simu: 026 23 21307
Nukushi: 026 23 21316